**Maana na maelezo kuhusu Uchaguzi Mdogo**

Uchaguzi Mdogo ni Uchaguzi unaofanywa angalau mara mbili kwa Mwaka ili kuwapata Viongozi wa kujaza nafasi zilizo wazi katika Kata au Majimbo kutokana na sababu mbalimbali. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 13 (1) na (3) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292 na kifungu cha 37 (1) (b) na (3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, miongoni mwa sababu hizo ni pamoja na;

- Mbunge, Diwani aliyekuwepo kufariki au kujiuzulu
- Mbunge, Diwani aliyekuwepo kukosa sifa ya kuendelea na nafasi yake kwa mujibu wa sheria
- Mahakama kutoa hukumu ya kubatilishwa kwa matokeo ya Uchaguzi.
- Ikiwa Mbunge, Diwani atajitoa au kuvuliwa Uanachama kutoka Chama kilichompa dhamana ya kugombea nafasi aliyonayo.

Aidha Uchaguzi Mdogo huratibiwa na kusimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi baada ya kupokea taarifa ya maandishi kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kuhusu uwepo wa nafasi wazi za Udiwani, au taarifa kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu uwepo wa nafasi wazi za Ubunge.

**Mambo yanayofanyika wakati wa Uchaguzi Mdogo**

Baada yakupokea taarifa ya uwepo wa nafasi wazi kutoka Mamlaka husika Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili kufanikisha Uchaguzi Mdogo hujishughulisha na mambo yafuatayo;

i. **Ratiba ya uchaguzi mdogo**

   Tume ya Taifa ya Uchaguzi hupanga Ratiba ya Uchaguzi Mdogo na kuwataarifu wadau wa Uchaguzi na Wananchi kwa ujumla kuhusu tarehe ya kutoa Fomu za Uteuzi, siku ya Uteuzi, Kampeni za Uchaguzi na Siku ya upigaji Kura.

ii. **Gharama za Uchaguzi**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi huandaa mchanganuo wa fedha na gharama zitakazotumika katika kukamilisha shughuli ya Uchaguzi Mdogo kulingana na idadi ya Vituo, Kata au Majimbo yanayotarajia kufanya Uchaguzi Mdogo.

iii. **Daftari la kudumu la wapiga Kura**

Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lilianzishwa chini ya Ibara ya 5(3) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Tume hutekeleza uandikishaji wa wapiga Kura chini ya Ibara ya 74 (6) (a) na (e) ya Katiba, aidha pale unapotokea Uchaguzi Mdogo wa Madiwani na Wabunge, Daftari linalotumika ni lile lililotumika katika Uchaguzi Mkuu uliopita ikiwa ni kabla ya uboreshaji wa Daftari hilo. Mfano Uchaguzi Mdogo wa 22 Januari 2017 lilitumika Daftari la Uchaguzi Mkuu wa 2015.

iv. **Vituo vya kupigia Kura**

Katika Uchaguzi Mdogo, Vituo vilivyotumika katika Uchaguzi Mkuu uliopita, ndivyo hutumika katika Uchaguzi Mdogo wa Madiwani na wabunge isipokuwa pale kituo kinapokuwa na tatizo na ikatakiwa kituo hicho kubadilishwa au vituo kuongezwa.

v. **Ununuzi wa vifaa vya Uchaguzi Mdogo**

Ununuzi wa vifaa kwa ajili ya Uchaguzi Mdogo hufanywa na Tume kwa kufuata Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 na Kanuni zake za Mwaka 2013. Vifaa kwa ajili ya Uchaguzi Mdogo ni pamoja na machapisho ya fomu mbalimbali zilizotumika wakati wa Uteuzi wa Wagombea, Vitabu vya Maelekezo, Sheria na Kanuni za Uchaguzi, Shajala na Mabango kwa ajili ya utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura na mafunzo ya watendaji na wakati wa Upigaji Kura. Nyaraka nyingine ambazo hununuliwa ni pamoja na fomu za matokeo, mfano wa Karatasi za Kura na Karatasi halisi za Kura.

vi. **Elimu ya Mpiga Kura**

Tume hutoa Elimu ya Mpiga Kura kwa mujibu wa Kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343. Katika kuhakikisha Elimu ya Mpiga Kura inawafikia Wapiga Kura wote, Tume hutumia njia mbalimbali za kufikisha

Elimu hiyo kupitia vipindi vya Redio za kijamii, Vipindi vya Runinga , Mitandao ya Kijamii na Tovuti.

vii. **Uteuzi wa watendaji wa uchaguzi**

Kwa Mujibu wa Vifungu vya 7 (1), 7 (2) na 8 (1) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Vifungu vya 9 (1) na 9 (2) vya Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume hufanya Uteuzi wa Watendaji wa Uchaguzi watakaosimamia shughuli za Uchaguzi katika ngazi za Mkoa, Halmashauri, Jimbo, Kata na Vituo vya Kupigia Kura ambao niWaratibu wa Uchaguzi wa Mikoa, Wasimamizi waUchaguzi wa Jimbo, Maafisa Uchaguzi ,Wasimamizi Wasaidizi Wawili ngazi ya Jimbo,Msimamizi Msaidizi mmoja kwa kila Kata,Msimamizi mmoja kila kituo;Wasimamizi Wasaidizi Wawili wa Kituo, Karani Mwongozaji wa Wapiga Kura mmoja, Mlinzi mmoja, Wasimamizi Wasaidizi wa Kituo wa akiba wawili kwa kila Kata, naMakarani Waongozaji Wapiga Kura wa akiba wawili kila Kata.

viii. **Mafunzo kwa watendaji wa Uchaguzi**

Katika kuhakikisha Uchaguzi Mdogo unasimamiwa na kuratibiwa kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu, Tume ya Taifa ya Uchaguzi hutoa mafunzo kwa watendaji wa Uchaguzi,Mafunzo hayohuhusisha Wasimamizi wa Uchaguzi, Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Jimbo, Maafisa Uchaguzi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kata.

ix. **Ugawaji na usambazaji wa Vifaa**

Tume hufanya usambazaji wa vifaa vya Uchaguzi Mdogokwenda kwenye Halmashauri zinazohusika katika Uchaguzi huo aidha miongoni mwa vifaa hivyo ni pamoja na fomu za Uteuzi, Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na Orodha ya Wapiga Kura, vifaa vya mafunzo kwa Watendaji wa Uchaguzi ngazi ya Kata na Vituo vya kupigia Kura, karatasi za mfano wa Kura, vituturi, betri, kangavuke na shajala, karatasi za Kura, fomu za matokeo, mhuri wa kituo na wino maalum.

x. **Uteuzi wa Wagombea na Kampeni za Uchaguzi**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi hutangaza tarehe ya Uteuzi wa Wagombea wa Uchaguzi ambao wanakuwa wamependekezwa na Vyama vyao na kutakiwa

kuwasilisha Fomu za Uteuzi katika Ofisi za Tume kabla ya muda uliopagwa siku hiyo ya Uteuzi. Hata hivyo, Tume hutoa nafasi kwa Wagombea kuleta Fomu zao siku tatu kabla ya Siku ya Uteuzi kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi kwa ajili ya kukaguliwa na kuona kama zimekidhi vigezo na masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria. Hii hutoa nafasi kwa Wagombea kuhakikiwa Fomu zao ili kama zina dosari wapate fursa ya kurekebisha kabla ya Siku ya Uteuzi.

xi. **<u>Ratiba na uratibu wa Kampeni</u>**

Kwa mujibu wa kanuni ya 39 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za Mwaka 2015, kipindi cha Kampeni kinaanza siku moja baada ya Siku ya Uteuzi wa Wagombea na kuishia siku moja kabla ya Siku ya Uchaguzi.Vyama vya Siasa vinavyokuwa na Wagombea wa nafasi ya Ubunge na Udiwani huandaa ratiba za kampeni na kuziwasilisha kwa Wasimamizi wa Uchaguzi/Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Jimbo na Kata kwa ajili ya uratibu wakati wote wa kipindi cha kampeni. Kwa kuzingatia kanuni ya 40, 41, 42, 43 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2015, na Kanuni ya 35, 36 na 37 ya Kanuni za Uchaguzi wa Madiwani za mwaka 2015, Msimamizi wa Uchaguzi ngazi ya Jimbo ni Msimamizi na Mratibu wa ratiba ya Kampeni za Uchaguzi wa Wabunge na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kata ni Msimamizi na Mratibu wa Kampeni za Uchaguzi wa Madiwani

xii. **<u>Kupiga na kuhesabu kura</u>**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia matakwa ya vifungu cha 55 na 56 vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 pamoja na vifungu vya 56 na 57 vya Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292 Tume hutangaza siku ya kupiga Kura kwa ajili ya Uchaguzi wa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Madiwani kwa Tanzania Bara na utaratibu mzima wa upigaji Kura.Kwa mujibu wa kifungu cha 70A(1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 70A(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292, kura za Rais, Mbunge na Diwani zitahesabiwa katika kituo kilichotumika kupigia Kura.

**xiii.** **Kujumlisha na kutangaza matokeo**

Aidha, kwa kuzingatia kanuni ya 55 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Madiwani) za mwaka 2015, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi baada ya kupokea matokeo ya Kura za Udiwani kutoka katika Vituo vyote ndani ya Kata husika, atavitaarifu Vyama vya Siasa au Mgombea tarehe, muda na mahali pa kujumlishia Kura za Udiwani. Kwa mujibu wa kanuni ya 61 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2015, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi baada ya kupokea matokeo ya Kura za Rais na Ubunge kutoka katika Vituo vyote katika jimbo husika, atavitaarifu Vyama vya Siasa au Mgombea tarehe, muda na mahali pa kujumlishia Kura.